

LAIKIPIA



UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

**1<sup>ST</sup> SEMESTER 2025/2026 ACADEMIC YEAR**

**SECOND YEAR EXAMINATIONS FOR THE  
DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION  
(ARTS)**

**KISW 211: ISIMUJAMII**

***STREAM: R***

***TIME: 2 HRS***

***DAY: THURSDAY (8.30-10.30AM)***

***DATE: 5/2/2026***

**THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF THREE (2 PAGES)**

**PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.**

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Jibu maswali **MATATU PEKEE. SWALI LA KWANZA** ni la lazima.
2. Hakikisha umeandika nambari yako ya usajili kwenye kila ukurasa.

**SWALI LA KWANZA (LAZIMA) – (Alama 20)**

- (a) Eleza uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii. **(alama 6)**
- (b) Jadili uhusiano kati ya isimu jamii na taaluma tatu zifuatazo: sosholojia, antropolojia, na siasa. **(alama 6)**
- (c) Jadili dhana ya lugha kama kioo cha jamii. **(alama 4)**
- (d) Kiswahili ni lugha sambazi na lugha rasmi nchini Kenya. Eleza **(alama 4)**

**SWALI LA 2 (Alama 20)**

- (a) Eleza jinsi jamii inavyoathiri muundo, matumizi na maendeleo ya lugha. **(alama 6)**
- (b) Kwa kutumia mifano, fafania dhana za vilugha, mitindo ya usemi, na sajili. **(alama 6)**
- (c) Kwa kutumia mifano, eleza nafasi ya lugha kama zana ya kitambulisho cha kijamii na kiutamaduni. **(alama 8)**

**SWALI LA 3 (Alama 20)**

- (a) Jadili changamoto zinazokabili uteuzi wa lugha katika elimu nchini Kenya. **(alama 6)**
- (b) Jadili mchango wa lugha ya kwanza katika elimu na maendeleo ya kijamii. **(alama 6)**
- (c) Eleza nafasi ya Kiswahili kitaifa na kimataifa, ukitathmini changamoto za upangaji lugha nchini Kenya. **(alama 8)**

**SWALI LA 4 (Alama 20)**

- (a) Eleza maana ya mielekeo kuhusu lugha na taja aina kuu za mielekeo hiyo katika jamii. **(alama 6)**
- (b) Jadili namna jinsia na mamlaka zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii. **(alama 6)**
- (c) Mitazamo ya kijamii kuhusu lugha inaakisi mienendo ya kijamii na kitamaduni. Eleza kuitumia mifano. **(alama 8)**

**SWALI LA 5 (Alama 20)**

- (a) Eleza tofauti kati ya sera ya lugha na upangaji lugha. **(alama 6)**
- (b) Ifanue historia ya sera za lugha nchini Kenya. **(alama 6)**
- (c) Jadili nafasi ya sera za lugha katika utawala, elimu, na siasa za Kenya. **(alama 8)**